# Sauti ya
Manispaa ya Morogoro



09



21



19



11



# Jarida la Mwezi
Mwezi Machi 2023
Toleo namba 09

# NDANI *ya Jarida*



16


03 Wanufaika wa Mikopo isiyo na Riba watakiwa kufanya Miradi yenye Tija ili kuweza kufanya Marejesho.

07 Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro ataka Jamii kupinga Ukatili wa aina zote ili kufikia Malengo ya kuwa na Kizazi chenye Usawa .

11 ununuzi wa vyeo sekta ya elimu, tabia hiyo haikubaliki-waziri kairuki.

19 Kamati Ndogo ya Afya Manispaa ya Morogoro yaridhishwa na Kasi ya Miradi ya Afya

21 Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro aahidi kutatua Kero Kichefuchefu ndani ya Manispaa.

23 Kamati Ndogo ya Mazingira Manispaa ya Morogoro yafanya Ziara, Diwani Kilongo atoa Mkono wa Pole kwa Waanga wa Mafuriko

28 zaidi ya vitabu 45,486 vya kabidhiwa kwa waalimu wa shule za msingi manispaa ya morogoro.




13

## yaliyomo


**06** **Manispaa ya Morogoro yaadhimisha Miaka 61 ya Uhuru, Msulwa ahimiza Wananchi kulinda Amani.**

**10** **Manispaa ya Morogoro Yaadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani, DAS Morogoro awaasa wananchi waishio na VVU kuendelea kutumia dawa za kufubaza Virusi.**

**14** **Kamati ya Kudhibiti UKIMWI Manispaa ya Morogoro yaahidi Kuboresha Mipango Kazi Ngazi ya Kata**


**17** **Waziri Mabula aagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza nguvu katika kukamilisha Zoezi la Urasimishaji**




24



26



# BODI YA UHARIRI


**Mhariri Mkuu ...** **Lilian K. Henerico**
*Afisa Habari Manispaa*

## Washiriki wasaidizi

**Neema Mwambi:** *Afisa Habari Msaidizi*
**Issa B. Issa:** *Afisa Habari Msaidizi*
**Yusuph Mwamba:** *Afisa Habari Msaidizi*
**Hajra Hashim:** *Afisa Habari Msaidizi*



*mawasiliano:* *simu: 023 - 2935242*
*E-mail: info@morogoromc.go.tz*
*S.L.P 166*


*Mitandao ya Kijamii*

| | |
|---|---|
| *Website:* | *www.morogoromc.go.tz* |
| *youtube:* | *Moromc online tv* |
| *instagram:* | *Manispaa ya Morogoro* |
| *facebook:* | *Manispaa ya Morogoro* |



*Wakufunzi wakiendelea na mafunzo kwa wawakilishi 87 ambao ni Makatibu , wenyeviti na waweka hazina wa Vikundi 29 vinavyotakiwa kupata mkopo.*

# WANUFAIKA WA MIKOPO ISIYO NA RIBA WATAKIWA KUFANYA MIRADI YENYE TIJA ILI KUWEZA KUFANYA MAREJESHO.

Wanufaika wa mikopo isiyo na riba ya asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotolewa na halmashauri kwa vikundi vya vijana, wakina mama na watu wenye Ulemavu Manispaa ya Morogoro wametakiwa kufanya shughuli za uzalishaji zenye tija na zitakazoleta faida ili kupata faida na kumudu kurejesha mikopo hiyo.

Rai hiyo imetolewa Desemba 29/2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano Ofisi Kuu na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Faraja Maduhu, wakati wa kufungua mafunzo kwa wawakilishi 87 ambao ni Makatibu , wenyeviti na waweka hazina wa Vikundi 29 vinavyotakiwa kupata mikopo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Akizungumza na wanavikundi hao, Maduhu, amebainisha kuwa ni vema kila kikundi kujikita kwenye shughuli za mradi ambao mmewasilisha kwenye andiko na kusimamia mradi huo ili uweze kuleta faida kwa manufaa ya familia na kurejesha deni pia.

Maduhu, amesema kuwa, ni muhimu kila mwanakikundi kutambua masharti ya mkopo unaotolewa na Serikali ya Awamu ya sita chini ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kuwajibika ipasavyo kufanya shughuli za miradi iliyokusudiwa ili fedha hizo ziweze kurudishwa kwa wakati na kusisitiza utunzaji wa kumbukumbu za matumizi yote ya fedha ili kuepuka upotevu wa fedha za Serikali.

“Mikopo hii inatolewa kwa watu waliokidhi vigezo kulingana na kiasi cha fedha kilichopo na si vinginevyo, ninyi mna sifa na mmekidhi vigezo vya kupata mkopo huu, niwaombe kuepuka matumizi yoyote yasiyo ya lazima ili muweze kufikia malengo yenu na kurejesha fedha hizo kwa wakati.” Alisisitiza Mvaa.

Naye Afisa Maendeleo ya Jamii , ambaye ni mwezeshaji wa elimu ,Joyce Mugambi, amesema kuwa lengo la Serikali kutoa mikopo hiyo isiyo na ribariba, walemavu, vikundi vya vijana na akinamama ni kutoa fursa kwa jamii kuinuka kiuchumi kupitia shughuli mbalimbli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kuzakuza ajira hasa kwa vijana ambao wanapitia changamoto ya kukosa mitaji ya kuanzisha biashara.

Kwa upande wa Mwezeshaji mwengine kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii, Josephine Mkuli, amesema Fedha hizo sio kwa ajili ya kugawana kwa kila mwanakikundi na kila mtu kufanya mradi anaotaka bali ni kwaajili ya kufanya mradi uliokusudiwa na wanakikundi wote kwa pamoja na faida itakayopatikana ndiyo inapaswa kugawanywa kwa kila mwanakundi.

wanufaika hao wameishukuru Serikali ya Awamu ya sita, inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwajali, wananchi wake na kuwapatia fursa nyingi za kujikwamua kiuchumi pamoja na kuzalisha ajira kwa watanzania waliokuwa wamekata tamaa ya kujiendeleza, kiuchumi kutokana na kukosa mitaji ya kufanyia biashara.







# Pochi la Mama lakimbiza Ujenzi wa Madarasa 81 Mapya   Manispaa ya Morogoro.

Hivi  karibuni Manispaa imepokea tena kiasi cha Shilingi bilioni 1.620,000  kupitia pochi la mama kwa ajili ya  ujenzi wa vyumba vya  madarasa.

Fedha hizo zimetolewa kwa mwezi Septemba kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 ya kidato cha kwanza watakaoingia mwakani 2023.

Katika fedha hizo ambazo Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amezitoa kwa ajili ya Ujenzi wa madarasa,, Manispaa ya Morogoro imeunga mkono juhudi za Mhe. Rais kupitia mapato yake ya ndani imeweza kuongeza madarasa 2 na kufanya jumla ya madarasa 83 ambayo asilimia kubwa ya   madarasa pamoja na Meza na viti vimekamilika.

Kwa takwimu hizo, ujenzi wa vyumba vya madarasa 83 vimegharimu kiasi cha shilingi Bilioni 1 na milioni 660.

Hii ni mara ya pili kupokea fedha ,ikumbukwe Manispaa ilipatiwa kiasi cha Shilingi Bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 86 ya Uviko 19




*Afisa Tawala Wilaya ya Morogoro, Hilary Sagara (kushoto) akimkabidhi Kishikwambi Diwani wa Kata ya Mlimani, Mhe. Zinduna Kombo , wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya matumizi ya vishikwambi kwa Madiwani, Wakuu wa Divisheni na Vitengo Manispaa ya Morogoro.*

# MANISPAA YA MOROGORO KUJIENDESHA KIJIGITALI, MADIWANI , WAKUU WA DIVISHENI WAKABIDHIWA VISHIKWAMBI.



*Madiwani wakiendelea na mafunzo ya matumizi ya Vishikwambi.*

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imefanya maboresho makubwa katika mfumo wa kujiendesha kisasa wa kutumia Vishikwambi kwa lengo la uwasilishaji wake wa taarifa hususani katika Vikao vya Mabaraza ya Madiwani.

Uzinduzi huo wa mafunzo ya Vishikwambi umefanyika Desemba 16/2022 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi Kuu ya Manispaa.

Akizungumza katika uzinduzi wa mfumo wa kijigitali mara baada ya kugawa Vishikwambi kwa Madiwani na Wakuu wa Divisheni na Vitengo , Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Hilary Sagara, amesema matumizi ya Vishikwambi yanalenga kuongeza ufanisi wa kazi na kuokoa fedha ambazo zimekuwa zikitumiwa kuchapisha makabrasha.

Sagara, amesema faida nyengine ya Manispaa kujiendesha Kijigitali ni kusaidia kuokoa muda wa kuandaa makabrasha ya Madiwani wakati wa vikao.

" Nichukue nafasi hii kuwapongeza Manispaa ya Morogoro kwa kuja na mpango bora wa mapinduzi ya kijidigitali, dunia sasa ipo Kijidigitali, vishikwambi hivi vitasiaida kuokoa fedha za machapisho ya makabrasha ambapo fedha hizo zinaweza kuelekezwa katika matumizi mengine ya maendeleo " Amesema Sagara.

Kwa upande wa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amewataka Madiwani kuwa waangalifu na vifaa hivyo na kuvitumia kwa matumizi yaliyokusudiwa ili viendelee kuwasaidia.

Naye , Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, amesema uwepo wa vishikwambi utarahisisha taarifa kufika kwa wakati kwa walengwa.

Katika hatua nyengine, Diwani wa Viti Maalum , Grace Mkumbae, amempongeza Mstahiki Meya kwa kuja na wazo hilo pamoja na wataalamu kwa kufanikisha mapango wa Manispaa kujiendesha kisasa.

# MANISPAA YA MOROGORO YAADHIMISHA MIAKA 61 YA UHURU, MSULWA AHIMIZA WANANCHI KULINDA AMANI.

MANISPAA ya Morogoro imeadhimisha sherehe za miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa kuandaa Kongamano la kujadili Maendeleo Endelevu ambayo Manispaa imeyapata katika kipindi cha Miaka 61 ya uhuru. Kongamano hilo limefanyika Desemba 09/2022 katika Ukumbi wa Mikutano Ofisi Kuu ya Manispaa ambapo mgeni rasmi akiwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Bakari Msulwa ambaye ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Kongamano hilo.

Akizungumza katika kongamano hilo, Mhe. Msulwa, alieleza kuwa ratiba hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mikoa na wilaya zote kuadhimisha sherehe za miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa kuandaa makongamano.

Katika Kongamano hilo, Mhe. Msulwa, amehimiza Wananchi kudumisha umoja na kulinda amani ya nchi kwa maendeleo Endelevu.

Msulwa, amesema kuwa,Tanganyika ilipata Uhuru Mwaka 1961 kwa amani bila umwagaji damu,hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuilinda amani ya nchi na kudumisha umoja ili nchi yetu iwe na maendeleo endelevu.

Naye Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Ruth John, amesema Kongamano hilo limelenga kuwakumbusha wananchi kuwa wanapaswa kujivunia amani waliyonayo kwani katika kipindi chote tangu kupatikana kwa uhuru hakujawahi kutokea machafuko kama ilivyo kwa maeneo mengine.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amesema katika kipindi cha miaka 61 ya Uhuru Manispaa inaendelea kukua kwa kasi kwani miradi mingi imekuwa ikitekelezwa kupitia fedha za ruzuku na fedha za mapato ya ndani.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, amesema Manispaa itaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi na kuimarisha pamoja na kuoboresha huduma zote muhimu ikiwamo huduma ya Maji, Umeme, Miundombinu ya afya na Barabara , Masoko pamoja na huduma za kijamii.

Katika hatua nyengine, aliyekuwa Katibu wa kwanza wa TANU Mkoa wa Morogoro, Mzee Juma Salumu Digallu, aliwashukuru waandaji wa kongamano hilo na kusema limewakumbusha wapi wametoka na wapi walipo na kuipongeza serikali kwa jitihada kubwa inayofanya kuleta maendeleo nchini.

Digallu, ameshauri Manispaa kuweka alama yoyote itakayotambulisha kuenzi mchango wa Mwalimu Nyerere katika kupiganía maendeleo ya Mkoa wa Morogoro kwa kuanzisha Viwanda vilivyokuwa ni sehemu ya ajira ya wananchi wa Morogoro akiwa Mbunge wa Kwanza wa Jimbo la Morogoro Mjini .



*Viongozi wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumalizika kwa Kongamano la kumbukizi la miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika la kujadili maendeleo endelevu yaliyofikiwa na Manispaa ya Morogoro.*

# MKURUGENZI MANISPAA MOROGORO ATAKA JAMII KUPINGA UKATILI WA AINA ZOTE ILI KUFIKIA MALENGO YA KUWA NA KIZAZI CHENYE USAWA .

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, ameitaka jamii kuhakikisha inapinga ukatili wa aina zote ili kufikia malengo ya kuwa na kizazi chenye usawa kati ya wanawake na wanaume.

Kauli hiyo ameitoa hivi karibuni , ikiwa ni kuelekea kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ambapo kilele chake kitafanyika Desemba 10/2022.

Akizungumza kuelekea kilele cha Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia , Machela, amesema kuwa maswala ya ukatili wa kijinsia yanaleta madhara makubwa katika jamii yasipo shughulikiwa ipasavyo,hivyo kila mwana jamii anawajibu wa kuhakikisha ukatili wa kijinsia unatokomezwa kwa kutoa taarifa kwenye vyombo husika kwa hatua zaidi.

Machela, emesema Manispaa imejipanga kupambana na ukatili wa kijinsia kwa kuanza kupita kwenye mitaa na kata kwa maeneo yote ya Magulio, vituo vya usafiri na nyumba za ibada kwaajili ya kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia.

" Ukatili wa kijinsia ni moja kati ya vitu vinavyopelekea mipango na ndoto za watu wengi hususani wanawake na watoto kushindwa kufikia ndoto zao hivyo ameiasa jamii kuacha vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto" Amesema Machela.

Katika kuona wanawake wanajikomboa kiuchumi na kuepukana na matendo ya ukatili dhidi yao , amesema kuwa Manispaa ya Morogoro, imeendelea kutenga fedha za asilimia 10 katika mapato yake ya ndani kuwawezesha kiuchumi wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kwa kutoa mikopo isiyo na riba pamoja na kuwapatia mafunzo ya stadi za biashara kwa wajasiriamali.

Kauli mbiu ya Siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia mwaka 2022 " kila uhai una thamani tokomeza mauaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto’’















*Picha za matukio mbalimbali ya maandamano katika maadhimisho ya siku ya wanawake duniani kata ya kihonda yaliyofanyika Machi 04/2023 ambapo katika maadhimisho hayo mgeni rasmi alikuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro Mhe. Norah Mzeru.*

*Picha mbalimbali zikionesha matukio ya uzinduzi wa mafunzo maalum ya uigizaji kwa Wasanii wa Mkoa wa Morogoro ambapo Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mh. Rebeca Nsemwa alikuwa mgeni rasmi katika mafunzo hayo yaliyofanyika Machi 03/2023 katika ukumbi wa soko la kingalu Mjini Morogo.*









# MANISPAA MOROGORO YAADHIMISHA SIKU YA UKIMWI DUNIANI, DAS MOROGORO AWAASA WANANCHI WAISHIO NA VVU KUENDELEA KUTUMIA DAWA ZA KUFUBAZA VIRUSI.

Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro ,Ruth John akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Manispaa ya




*Wadau wa Ukimwi wakiwa katika maandamano ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Manispaa ya Morogoro yaliyofanyika Desemba 01/2022 katika Viwanja vya Chuo cha Mifugo Liti Kata ya Mlimani.*

Morogoro, amewaasa Wananchi wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kuendelea kutumia dawa za kufubaza virusi hivyo ili waweze kuishi maisha yenye afya na amani wakati wote.
Ametoa kauli hiyo wakati akizungumza na wananchi waliojitokeza katika Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Manispaa ya Morogoro iliyofanyika Desemba 01/2022 katika Viwanja vya Chuo cha Mifugo Liti Kata ya Mlimani.
Akizungumza katika maadhimisho hayo, Bi. Ruth , ameipongeza Manispaa ya Morogoro , wadau wa Ukimwi na kamati kwa kuandaa siku muhimu kama hiyo ambayo inalenga kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi.
“Kipekee ninawapongeza kwa ujasiri wenu wale ambao wamekuwa wakijotokeza kupima na kukutwa na maambukizi, janga hili lipo na ni letu sote, kwani naamini hakuna mtu ambaye halijamgusa kwa namna moja au nyingine hivyo niwaombe wale ambao wamegundulika na maambukizi wajitahidi kuendelea kutumia dawa za kufubaza makali ya virusi ili kuendelea kuimarika zaidi,na wale wasio na maambukizi waendelee kujilinda wao pamoja na familia zao ”Amesema Ruth.
Aidha,Bi. Ruth, amesisitiza wale ambao hawana maambukizi waendelee kuwa mabalozi wazuri kwa wengine juu ya maambukizi na wale ambao hawajatambua hali zao na wale waliotambua hali zao kuendelea kutumia dawa zakufubaza virusi na kutoacha kutumia dawa hizo kwa kuzingatia umuhimu wake.
Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amewataka wenye maambukizi wasiache wala kuchoka kutumia dawa hizo kwani kwa kuzingatia umuhimu wake zina wahakikishia na zinawapa nafuu na kuondoa magonjwa nyemelezi kuendelea kuwa na afya njema na kushiriki katika shughuli za kimaendeleo na kufanya dunia mahali salama pa kuishi.
“Serikali imejipanga kuhakikisha kundi la WAVIU wote wanahudumiwa na kupatiwa mahitaji yao muhimu ikiwemo upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya virusi (ARV) hivyo, hivyo ni vyema sasa Serikali na wadau tukaungana pamoja kuhakikisha maambukizi mapaya ya Ukimwi yanapungua badala ya kuongezeka" Amesema Mhe. Kihanga.
Kwa upande wa Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Faraja Maduhu, amesema maambukizi ya Ukimwi yamepanda kwa asilimia 1.0 ambapo mwaka Julai 2021 hadi Juni 2022 watu 62,010 walipima VVU kati ya hao wanawake 4,1351 , wanaume 20,659 na waliokutwa na Ukimwi ni watu 3,527 kati yao wanaume 1,481 na wanakae 2,046 sawa na asilimia 5.6 mwaka 2021/2022 kutoka asilimia 4.6 ya mwaka 2020/2021.
Kamati ya kudhibiti Ukimwi ikiongozwa na Naibu Meya wa Manispaa ya Morogoro ambaye ni Diwani wa Kata ya Sabasaba ,akiwa na wajumbe wake waliohudhuria maadhimisho hayo pamoja na Diwani mwenyeji wa Kata ya Mlimani Mhe. Zinduna.



*Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro, Ruth John,(watatu kutoka kulia) akisalimiana na wadau wa Ukimwi katika Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Manispaa ya Morogoro yaliyofanyika Desemba 01/2022 katika Viwanja vya Chuo cha Mifugo Liti Kata ya Mlimani.*

# UNUNUZI WA VYEO SEKTA YA ELIMU, TABIA HIYO HAIKUBALIKI-WAZIRI KAIRUKI.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,(TAMISEMI), Angellah Kairuki amewaonya watumishi katika sekta ya elimu wanaodaiwa kutumia madaraka yao kwa kutoa vyeo kwa misingi ya Rushwa kuacha mara moja kabla hawajabainika na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Waziri Kairuki alisema hayo Januari 9, 2023 mjini Morogoro wakati akifungua kikao kazi cha mapitio ya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu kwa mwaka 2022 na mpango mwaka 2023.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,(TAMISEMI), Angellah Kairuki , akizungumza na wadau wa elimu katika ufunguzi wa kikao kazi cha mapitio ya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu kwa mwaka 2022 na mpango wa mwaka 2023 uliofanyika Manispaa ya Morogoro Januari 9, 2023.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,(TAMISEMI) Angellah Kairuki, akizungumza na Watendaji wa Idara ya Elimu ngazi ya mkoa na Halmashauri Januari 9, 2023 mjini Morogoro wakati akifungua kikao kazi cha mapitio ya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu kwa mwaka 2022 na mpango mwaka 2023.*

Waziri amesema wapo baadhi ya watumishi wa sekta ya elimu wanaodaiwa kutoa rushwa ili kupata madaraka ya Ofisa elimu wa wilaya na ngazi nyingine jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kiutumishi na ni kosa kisheria.

Kairuki amesema hategemei endapo mkuu wa shule amepata cheo hicho kwa kutoa rushwa kwani hataweza kufanya kazi kwa uadilifu, kwa maana lazima atafanya kila njia ili aweze kurejesha kile alichotoa.

" Nasema kama mambo haya yapo yakome mara moja, Serikali ipo makini, hatutawafumbia macho wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivi na kwamba wakibainika watachukuliwa hatua kali za kisheria "amesema Waziri Kairuki

Waziri amesema kwa upande wa viongozi kuna nyakati wamepewa madaraka ya kukathimisha uongozi na kupendekeza wanaostahili kushika nafasi mbalimbali za uongozi na kuwataka kuwa macho.

“ Tumetoa mwongozo wa teuzi mbalimbali katika sekta yetu ya elimu katika mamlaka za Serikali za mitaa , ni vema tukafuata miongozo hiyo” amesema Waziri

Waziri amesema zipo tuhuma au yako maneno ya kwamba wengine wameingia kama maofisa elimu kwa kutoa rushwa , wapo wengine wamepata ukuu wa shule kwa kutoa fedha.

“Tutaendelea kuyangalia kwa umakini mkubwa,tunataka mtu anayepata nafasi ya uongozi awe ni yule kweli ni mahili yule anayekidhi vigezo vyote vilivyowekwa” amesema Kairuki

Pia amesema yako maneno ya kwamba wako baadhi ya maofisa elimu ili aweze kuteua baadhi ya wakuu wa shule ukipewa nafasi lazima watoe fedha na kila mwezi wanapekelewa fedha .

“ Kama yapo hayo kwa maofisa elimu yakome , kwa wakuu wa shule yakome na ikitokea wewe mkuu wa shule unashinikizo la kutoa fedha kwa yoyote …nitaancha namba zangu hapa tafadhari usisite kuweza kutoa taarifa na tutawalinda’ amesema Waziri

Waziri amesema Ofisi yake ipo macho na kwamba mabadiliko mengi yataendelea kufanyika na pia hatua zitachukuliwa za kisheria na hata za kijinai zitachukuliwa dhidi ya hao na kutoa rai kama wapo mambo hayo yakome.

Waziri pia amewatahadharisha watumishi wa umma wanaokiuka taratibu na kanuni za kiutumishi kwa kutoa lugha chafu kwa wananchi wanashungulikiwa kulingana na sheria za kinidhamu na kwamba itawekwa mitego kila sehemu zinapotolewa huduma za kijamii kwa watawatega kwa maswali ili mjibu lugha chafu tuwabaini wenye tabia za kutoa lugha chafu ili tuwachukulia hatua.

*Picha za matukio mbalimbali ya maandamano katika maadhimisho ya siku ya wanawake duniani kata ya Mkundi yaliyofanyika Machi 04/2023 ambapo katika maadhimisho hayo mgenirasmi alikuwa Diwaniwa Kata ya Mkundi Mhe. Seif Chomoka.*
















Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Kingo, Mhe. Amini Tunda,akizungumza na wajumbe wa Kamati wakati wa ziara .

# KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI , ELIMU NA AFYA YAPONGEZA UJENZI MIRADI YA ELIMU NA AFYA KUKAMILIKA KWA WAKATI.

Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya Manispaa ya Morogoro imepongeza wataalamu pamoja na timu nzima ya Utawala ikiongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa kwa kukamilisha miradi ya elimu na afya kwa wakati , ikiwemo ujenzi wa madarasa ya Pochi la Mama.

Pongezi hizo zimetolewa Januari 19/2023 na kamati hiyo iliyoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Kingo, Mhe. Amini Tunda baada ya kukagua ujenzi wa madarasa ya shule za Sekondari na Msingi pamoja na miradi ya afya.

Akizungumza katika ziara hiyo juu ya ujenzi wa madarasa, Mhe. Tunda, amesema Manispaa ya Morogoro ilipokea Shilingi Bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 81 kupitia fedha zijulikanazo kama Pochi la Mama ikiwa na lengo la kuinua kiwango cha taaluma na kufuta machaguo ya kwanza, pili na tatu kama ilivyozoeleka hapo awali.

Amesema Serikali inawajali wananchi wa Manispaa ya Morogoro na kwamba wameitendea haki fedha ya Serikali lakini pia wamekamilisha kwa wakati na kazi yao kuwa nzuri hali inayoashiria hakuna hata mwanafunzi mmoja ambaye atashindwa kuwasili darasani na kuanza masomo kutokana na uhaba wa madarasa kwenye halmashauri hiyo.

Pia, Wajumbe wa Kamati hiyo wamepongeza timu ya Utawala ya Manispaa inayoongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa, Ally Machela, kwa kuongeza madarasa 2 kupitia mapato ya ndani na kuongeza madarasa katika fedha ya pochi la mama na kufanya jumla ya madarasa 83 jambo ambalo limeonesha jinsi gani Manispaa imeunga mkono juhudi za Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan , za kuboresha elimu kwani kazi za mapato ya ndani ni kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.



Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya Manispaa ya Morogoro, wakijadiliana jambo katika ziara ya kamati yao.

Mhe. Tunda, amesema kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Manispaa ya Morogoro kupitia mapato yake ya ndani kwa kipindi cha mwezi mmoja iliweza kukamilisha ujenzi wa madarasa 10 lengo likiwa ni kuongeza nguvu kwenye ujenzi wa madarasa.

Mwisho kamati hiyo, imeipongeza Menejimenti ya Manispaa kwa hatua nzuri ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya , kukamilisha ujenzi wa Zahanati 6 ambazo zote zimeanza kutoa huduma , ujenzi wa Vituo vya afya 2, Lukobe na Tungi ambavyo vipo katika hatua ya mwisho pamoja na Zahanati mpya ambazo ujenzi unaendelea.

Upande wa Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Jeremia Lubeleje, ameipongeza Serikali chini ya Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, .Dkt. Samia Suluhu Hassan kutoa fedha nyingi ili kujenga madarasa , ambapo awali aliipatia Manispaa Shilingi Bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 86 ya UVIKO-19.

# Maboresho makubwa kufanyika kwa Shule za Msingi Nchini.

Serikali imetenga kiasi cha Sh trilioni 1.15 kwa ya matumizi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya shule za msingi zilizochakavu kupitia Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST), katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka huu wa fedha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,(TAMISEMI) Angellah Kairuki, alisema hayo Januari 9, 2023 mjini Morogoro wakati akifungua kikao kazi cha mapitio ya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu kwa mwaka 2022 na mpango mwaka 2023.

Mpango wa ujenzi na ukaratabi wa miundombinu ya shule hizo unatarajia kuanza kutekelezwa Januari na Februari mwaka huu nchini kote.

Waziri alisema kuwa baadhi ya shule zitavunjwa na kujengwa upya ,nyingine zitafanyiwa ukarabati mkubwa pamoja na mdogo kwa lengo la kuzifanya ziwe na mazingira bora kulingana na hali ya sasa kwa walimu na wanafunzi.

Alisema Serikali inatambua shule nyingi ni za muda mrefu ambazo zilijengwa na Serikali, wadau na wazee na nyingine kwa njia ya kujitolea ambazo zimeweza kudumu kwa muda mrefu na imefika wakati sasa wa kuziboresha shule hizo.

Waziri alisema katika kuendelea kuimarisha elimu ya Sekondari kupitia mradi wa SEQUIP, ambapo Jumla ya sh trilioni 1.2 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 1,026 ( Za kata 1,000 na za bweni za wasichana za Mkoa 26) katika kipindi cha miaka mitano.

Waziri huyo alisema mwaka 2021 jumla ya shule mpya 232 za sekondari za Kata zimeshajengwa na 10 za bweni za wasichana za mikao zinaendelea kukamilisha ujenzi wake.

Alisema kwa mwaka 2022/23, Serikali inategemea kujenga shule mpya za Kata 184, moja kila Halmashauri na shule tano (5), za bweni za wasichana kwenye mikoa mitano.

Waziri pia alisema kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu Serikali itatoa sh milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa shule moja ya sekondari kwa kila Halmashauri nchini

“Nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Dk Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa hizi anazoendelea kuzifanya katika kuimarisha na kuboresha sekta ya Elimu nchini” alisema Kairuki

Kwa upande uandikishwaji wa wanafunzi wa darasa la awali na msingi nchini aliagiza watendaji wa sekta ya elimu , wakurugenzi wa Halmashauri , wakuu wa wilaya na mikoa kuongeza kasi ya kusajili wanafunzi ili kufikia malengo ya yaliyokusudiwa ya asilimia 100 .

“Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa muendelee kuhamasisha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali na msingi ili kuhakikisha mnafikia malengo ya uandikishaji mliyokuwa mmejiwekea” alisema Waziri Kairuki

Waziri Kairuki alisema “Kila kiongozi akahakikishe anaimarisha uwajibikaji wa watumishi wote katika ngazi zote ili kuongeza tija katika utendaji wa kazi” alisisitiza Waziri

Hivyo alisema natarajia kuanzia Januari 2023 kutakuwa na mabadiliko makubwa katika usimamizi wa elimu msingi na sekondari katika shule zetu.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Tamisemi, Vicent Kayombo alisema utekelezaji wa sera ya elimu bila ada imeongeza idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa kujiunga elimu ya awali, msingi na sekondari nchini

Kayombo alisema bado zipo changamoto kadhaa ikiwemo kwa wanafunzi wanao maliza darasa la saba hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu huku kukiwa na wanafunzi asilimia 20 wanaoshindwa kufaulu mtihani wa elimu ya msingi na kushindwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Pia alisema kumekuwepo na idadi ndogo kwa wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kidato cha nne kwa daraja la kwanza hadi tatu likiwemo somo la Kiingereza .

Kwa upande wake Mkuu wa mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa,katika taarifa yake kwa Waziri alisema kuwa ,wanafunzi walioandikishwa darasa la awali na msingi hadi kufikia Januari 6, mwaka huu walifikia 74,578 kati ya hao wavulana 37,342 na wasichana 37578 sawa na asilimia 94.5

## KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI MANISPAA YA MOROGORO YAAHIDI KUBORESHA MIPANGO KAZI NGAZI YA KATA

Kamati ya Kudhibiti Virusi vya Ukimwi na UKIMWI Manispaa ya Morogoro imesema kwa sasa watahakikisha wanaelekeza nguvu katika kuboresha mipango kazi ngazi ya Kata ili kudhibiti maambukizi mapya ya Ukimwi.

Kamati hiyo, imesema hayo Januari 23/2023, katika ziara ya kutembelea Kata ya Bigwa ambayo imeonekana kufanya vizuri katika maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yaliyofanyika Desemba 01/2022.

Akizungumza kwa niaba ya wajumbe wa Kamati hiyo, Mwenyekiti wa Kamati , ambaye ni Naibu Meya wa Manispaa ya Morogoro na Diwani wa Kata ya Sabasaba,Mhe. Mohamed Lukwele, amesema kumekuwa na kusuasua kwa maandalizi ya maadhimisho ya Ukimwi ngazi ya Kata, hivyo katika vipindi vijavyo watahakikisha wanafanya maboresho ya kuweka mikakati na mipango thabiti ya kuzipa nguvu



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti Ukimwi Manispaa ya Morogoro Mhe. Mohamed Lukwele, (katikati), Mratibu wa kudhibiti Ukimwi Manispaa ya Morogoro Upendo Elias (kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja katika ziara ya Kamati ya Ukimwi.*

kamati za Kata ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi.
" Leo tupo Kata ya Bigwa, wenzetu walifanya vizuri sana katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi ya mwaka 2022, Desemba ngazi ya Kata, kuna kila sababu ya kujifunza walifanikiwa vipi, niombe sana Kata nyengine wakati tunaelekea katika maadhimisho mengine ni vyema wakafika kujifunza lakini sisi kama Kamati tunaenda kuboresha na kuweka mipango yetu vizuri ya Kuongeza Bajeti , tunataka kamati zipewe umuhimu kulingana na majukumu wanayoyafanya ya kupunguza maambuziki mapya ya virusi vya UKIMWI" Amesema Mhe. Lukwele.
Pia, amewapongeza Viongozi Kata ya Bigwa kwa kufanikiwa kupunguza maambukizi ya watu wenye virusi vya Ukimwi, kwani takwimu imeonesha kutoka januari -Desemba , 2022 jumla ya waliopima walikuwa 195, ambapo katika idadi hiyo wanaume 87 na wanawake 108 katika Zahanati za Mgolole, Vituli na Misongeni.
Mbali na uhamasishaji wa watu kupima, mafanikio yao yalitokana na kuanzisha mradi wa TIMIZA MALENGO wenye lengo la mabinti wadogo kujiepusha kujiingiza katika masuala ya ngono wakiwa na umri madogo, ambapo katika mradi huo jumla ya Mabinti 133 walipatiwa elimu juu ya mradi huo.
Licha ya kuwa na mradi wa Timiza Malengo, Kata ya Bigwa walienda mbali zaidi na kuanzisha mradi ujulikano kama elimu bora kwa jamii ukiwa na lengo la kuielimisha jamii kuwa bora na kuwa na mtazamo chanya wa maisha.
Mwisho, Kamati hiyo imewataka wananchi kuwa na utaratibu wa kupima afya kwani kupima afya kuna faida ya Kujua afya zao na kuweza kupanga mipango yao , kunusuru afya ya mama na mtoto endapo ameathirika na kutoendelea kuambukiza na kupokea maambukizi mapya.



*Wajumbe wa Kamati yakudhibiti UKIMWI na UKIMWI , Mhe. Mathias Kanga (kulia), Mwanaidi Ngulungu.*



*Mratibu wa kudhibiti Ukimwi Manispaa ya Morogoro Upendo Elias, akizungumza na Wajumbe wa Kamati.*



# Manispaa ya Morogoro yakabidhi Vishikwambi 1259 kwa Waalimu wa Shule za Msingi na Sekondari. DC Msando ato neno.



*Picha katika matukio mbalimbali zikimuonesha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Albert Msando, akigawa Vishwikwambia kwa waalimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Ukumbi wa Mikutano Ofisi Kuu ya Manispaa Januari 19/2023.*

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Adv. Albert Msando , ameongoza zoezi la ugawaji vishikwambi 1259 kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari zilizopo Manispaa ya Morogoro.
Zoezi hilo limefanyika katika ukumbi wa mikutano Ofisi Kuu ya Manispaa ya Morogoro Januari 19/2023.
Akizungumza katika zoezi hilo , DC Msando, amewataka walimu kutunza zana hizo za kazi (vishikwambi) pamoja na kufuata maelekezo yote yaliyotolewa kutoka kwenye muongozo juu ya utunzaji na utumiaji.
“Tunakila sababu ya kuishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuboreshea miundombinu katika sekta ya elimu, nendeni mkavitumie vishikwambi (tablet) hivi kwa malengo yaliyokusudiwa, tumieni vishikwambi hivi katika mambo ya msingi kama kutumiana maswali, kapakua vitu mbalimbali vya ufundishaji mtandaoni lengo ni kuongeza ufaulu katika shule za Msingi na Sekondari. " Amesema DC Msando.
Aidha, amesema, vishikwambi hivyo vimeletwa kwa kwa ajili ya matumizi ya kujifunzia na kufundishia kwa walimu wa shule za Msingi na Sekondari na sio kwa matumizi mengine ,hivyo amewataka waalimu wakatekeleze utumiaji wa zana hizo kama masharti yalivyoelekezwa katika muungozo wa matumizi yake.
Naye Afisa Elimu Sekondari Manispaa ya Morogoro , Gabriel Paul, amesema kuwa upande wa Elimu Msingi jumla ya vishikwambi 893 vimegaiwa na upande wa Shule za Sekondari vimegaiwa vishkwambi 366.
" Niwaombe Waalimu kuzingatia usalama katika utunzaji wa vishikwambi hivyo na nitoe wito kwa waalimu wote waliopata vishikwambi hivyo waweze kushirikiana na wengine ambao hawajapata ili waendelee kuboresha ujifunzaji na ufundishaji shuleni" Amesema Gabriel.

# WAZIRI MABULA AAGIZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KUONGEZA NGUVU KATIKA KUKAMILISHA ZOEZI LA URASIMISHAJI



***Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Angeline Mabula, akizungumza katika kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa mpango kabambe wa urasimishaji makazi kilichofanyika Februari 22/2023 , Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi Kuu ya Manispaa ya Morogoro.***

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Angeline Mabula, ameziagiza mamlaka za Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi nchini kuhakikisha zinaongeza nguvu katika kukamilisha zoezi la urasimishaji wa makazi kabla ya kumalizika kwa mwaka 2023 ambao ndio mwisho wa zoezi hilo.

Waziri Mabula amesema hayo leo Februari 22/2023 katika kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa mpango kabambe wa urasimishaji makazi kilichofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi Kuu ya Manispaa ya Morogoro.

Akizungumza katika kikao hicho, Waziri Mabula, amesema kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa inayo jukumu la urasimishaji na upangaji wa miji kwa kushirikiana na Makampuni ya urasimishaji badala ya kuitegemea Wizara kutenga fedha hizo.

" Tumeweka mpango kabambe wa urasimishaji , mwisho mwaka huu 2023, niombe mamlaka za upimaji , usimamizi na uratibu wa ardhi mfanye kazi zenu ipasavyo, niombe mkasimamie vizuri upangaji wa miji ili kuepusha migogoro ya ardhi na kupanga miji vizuri, niwapongeze Manispaa ya Morogoro kwa kufika asilimia 53 ya urasimishaji katika Mkoa wa Morogoro " Amesema Waziri Mabula.

Katika hatua nyengine, amesema maeneo ambayo hayajaendelezwa yanachafua taswira ya Miji na yanapoteza mapato ambayo kama yangeendelezwa yangekuwa na faida kiuchumi, hivyo Viongozi wawaelimishe wananchi kuhusu mipaka ya ardhi pamoja na kuyaendeleza maeneo yao.

Miongoni mwa maagizo aliyotoa kwa Halmashauri nchini ni Halmashauri kukaa na Makapuni waliyoyapa tenda ya kazi ya urasimishaji kukaa nayo ili kuona namna gani gani kazi ambazo hawajakamilisha wanazikamilisha kikamilifu, Kampuni zitakazoshindwa kutekeleza zoezi hilo la urasimishaji wawafutie tenda na kudai fedha zao pamoja na kutokutoa tenda mpya kwa makampuni ambayo hayakumaliza kazi ya urasimishaji.

Dkt. Mabura, amesema , zipo hatua ambazo Wizara ya ardhi imezichukua ikiwemo Wizara kufanya kikao kazi na TAMISEMI kuona namna gani ya kushirikisha Halmashauri kutenga fedha katika Sekta ya ardhi juu ya upangaji na urasimishaji pamoja na kufanya kikao na Makampuni ya urasimishaji ili kuwapa mpango kazi wa utekelezaji wa zoezi la urasimishaji.

Hata hivyo, amesema zipo changamoto ambazo zimejitokeza katika kutofanya vizuri katika mpango kabambe ikiwemo kazi za urasimishaji kuchelewa au kutokukamilika, uchangiaji hafifu wa uchangiaji katika urasimishaji, usimamizi usiolizisha kwa mamlaka ya urasimishaji , baadhi ya Makampuni kuchukua pesa bila kumaliza kazi na kutokuwepo kwa kumbukumbu na nyaraka za mapato ya ukusanyaji wa fedha za urasimishaji.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi, Wizara ya ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratias Desderius , amesema asilimia 35 ya wananchi Tanzania wanaishi Mjini huku akisema ongezeko la watu ni asilimia 3.2 .

Amezitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza nguvu katika upangaji wa maeneo , kwani hali inaonesha zaidi ya miji 4310 imekuwa ikichipuka na kukuwa kutokana na Serikali kuboresha huduma za kijamii Vijijini na Mijini.

Amesema kuwa katika kuona zoezi la urasimishaji linafanikiwa , Wizara imeandaa muongozo wa uendelezaji wa nyumba Vijijini na Makazi bora.

Naye Afisa Mipango Miji Manispaa ya Morogoro, Emeline Kihunrwa, akiwasilisha mpango kabambe wa urasimishaji, amesema asilimia 65 limepimwa na asilimia 35 ya eneo lililopimwa bado barabara zake hazijafunguliwa.

Kihunrwa, ametaja mapendekezo ya mpango kabambe wa Halmashauri , miongoni mwa mapendekezo hayo ni kuanzisha vituo vya biashara nje ya mji, urasimishaji makazi holela, utunzaji wa vyanzo vya maji, uendelezaji wa mji, kuboresha mifumo ya maji taka na taka ngumu pamoja na kutenge maeneo ya maegesho.









# KAMATI NDOGO YA AFYA MANISPAA YA MOROGORO YARIDHISHWA NA KASI YA MIRADI YA AFYA

Kamati ndogo ya afya Manispaa ya Morogoro ikiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mhe. Aisha Kitime, imefanya ziara ya kukagua miradi ya afya inayotekelezwa katika Manispaa hiyo na kutoa pongezi za uendeshaji wa miradi kwa kuzingatia viwango ikiwemo ubora wa majengo pamoja na kasi ya uendeshaji.
Kauli hiyo ameitoa Januari 19/2023 wakati wa ziara ya kukagua miradi ya afya ikiwamo Zahanati na Vituo vya afya katika kuona huduma zinazozotolewa kwa wananchi.
Mhe. Kitime,amesisitiza muda uliopangwa wa uendeshaji wa miradi kukamilika uendelee kuzingatiwa na katika maeneo ambayo yameonekana kuna changamoto yafanyiwe kazi pamoja na kuboresha huduma za afya katika vituo hivyo.
"Tumetembelea miradi yetu ya afya, lengo la kamati hii ndogo ni kusaidia kamati kuu ya afya kufanya kazi kwa urahisi, ,tumeona ubora wa majengo ni mazuri na wauguzi wetu wanajitahidi kuwahudumia wagonjwa, kikubwa niombe kuwasisitiza waganga wafawidhi katika Vituo kuwashirikisha viongozi wenu wa ngazi ya kata kwenye Kila hatua kuepusha kutokea kwa changamoto mwishoni" Amesema Mhe. Kitime.
Mhe. Kitime, amewataka Waganga wafawidhi kuhakikisha katika vituo vyao kuna vifaa tiba vidogovidogo huku wakiendelea kusubiria vifaa vyengine vya huduma.
Mwisho wajumbe waliendelea kusisitiza katika changamoto zilizopatikana kwenye baadhi ya miradi kutiliwa mkazo kuhakikisha zinafanyiwa kazi ikiwa ni moja ya kazi ya kutimiza majukumu ya kamati.

Miradi iliyotembelewa na kamati ndogo ya afya ni Zahanati ya Kauzeni, Zahanati ya Konga Kata ya Mzinga, Zahanati ya Kata ya Kihonda, Zahanati ya Kata ya Chamwino pamoja na Zahanati ya Kata ya Lukobe.
Manispaa ya Morogoro kupitia mapato yake ya ndani imeshatekeleza ujenzi wa Zahanati 6 ikiwamo Mbuyuni, Kihonda Maghorofani, Sultan Area, Tungi, Mgaza Mindu, na Kiwanja cha ndege huku Zahanati nyengine zikiendelea na ujenzi.



***Jengo la Ujenzi wa Zahanati ya Kata ya Kauzeni linalojengwa kupitia fedha za mapato ya ndani.***



***Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya afya Manispaa ya Morogoro , Mhe. Aisha Kitime, akiongoza wajumbe wa kamati hiyo katika ziara ya kukagua miradi ya afya***

# ZAIDI YA VITAMBULISHO 83 VYAGAIWA KWA WAZEE KATA YA MAZIMBU MANISPAA YA MOROGORO.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, ambaye ni Diwani wa Kata ya Mazimbu , amegawa vitambulisho vya msamaha wa matibabu kwa wazee 83 katika kata hiyo kwa lengo la kuvitumia kwa ajili kutambulika na kupata huduma ya Afya bure katika hospitali za Serikali.

Zoezi hilo limefanyika Januari 19/2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Kata ya Mazimbu ambapo makabidhiano hayo yamefanyika kwa Wenyeviti wa Mitaa ya Kata hiyo yakishuhudiwa na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Kata ya Mazimbu Ndugu, Isack Wella.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa Vitambulisho hivyo, Mhe. Kihanga, amewahakikishia wazee hao kuwa zoezi hili ni endelevu kwa Kata zote 29 ili kuhakikisha kila mzee aliyoko ndani ya Manispaa ya Morogoro hii anapata kitambulisho hiko.

Naye Afisa Ustawi kutoka Ofisi ya Ustawi , David Max, amewataka wazee wote waliopata vitambulisho vya msamaha wa matibabu kuanza matibabu katika ngazi ya Zahanati zilizoko katika mitaa yao hadi ngazi ya Wilaya.

Akiongea mara baada ya zoezi la ugawaji wa vitambulisho hivyo, Mwenyekiti wa Wazee Kata ya Mazimbu, Isack Wella, amewaomba Madaktari na Wauguzi kutoa huduma hiyo bila kuwanyanyasa pamoja na kuiomba Serikali kuruhusu vitambulisho hivyo kutumika kwenye huduma zote kwa maana ya kupatiwa vipimo pamoja na Dawa.

Manispaa ya Morogoro ni mion-goni mwa Halmashauri zinazotekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungan wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha kuwa wazee wote wanapata Matibabu bure kupitia Vitambulisho hivyo vya Msamaha wa Matibabu.



***Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, ambaye ni Diwani wa Kata ya Mazimbu ,akigawa vitambulisho vya msamaha wa matibabu kwa wazee 83 katika kata hiyo kwa lengo la kuvitumia kwa ajili kutambulika na kupata huduma ya Afya bure katika hospitali za Serikali.***



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, akizungumza katika kikao cha Kawaida cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano Ofisi Kuu ya Manispaa Februari 08/2023.*

# MKURUGENZI MANISPAA YA MOROGORO AAHIDI KUTATUA KERO KICHEFUCHEFU NDANI YA MANISPAA.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, amewahakikishia wananchi wa Manispaa ya Morogoro kua hakutakua na kero babaifu za huduma za jamii kutokana na kuwepo kwa mikakati madhubuti iliyowekwa na halmashauri hiyo katika kutekeleza majukumu yake.

Ameyasema hayo Kupitia kikao cha Kawaida cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano Ofisi Kuu ya Manispaa Februari 08/2023.

Kupitia maswali yalioluizwa ya papo kwa papo na Madiwani wakipambania utatuzi wa changamoto zinazozikabili kata zao,Machela, amewatoa hofu Madiwani kwa kusema kuwa Manispaa ina mipango mizuri na utekelezaji utaanza mara moja kwakua fedha za halmashauri zipo za kutosha.

Katika upande wa elimu , Machela, amewataka wananchi kuendelea kujitolea na kufanikisha upatikanaji wa maboma kwa ajili ya Madarasa na Serikali itamalizia kwa sehemu iliyobaki kwa asilimia miamoja ikiwa ni pamoja uezekaji na upatikanaji wa madawati.

Pia amewahakikishia kua swala la upungufu Madawati linakwenda kuisha hivi karibuni kwakua ni kipaumbele cha kwanza katika bajeti ya robo ya tatu inayoanza hivi karibuni, jumla ya shilingi 500 zimetengwa kwa ajili ya Madawati.

Kuhusu huduma ya afya, Machela, amesema mpango uliokuwepo ni kuhakikisha wanajenga majengo mawili makubwa ya Upasuaji katika Kituo cha afya Mafiga na Sabasaba.

“Tutaendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi wetu, mkakati wetu ni ujenzi wa majengo ya upasuaji, lakini suala la changamoto ya vifaa tiba katika Zahanati zetu, hilo tumeliona na Manispaa imetenga fedha kidogo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa ambapo hivi karibuni tutaanza kusambaza huku tukisubiria vifaa vingine toka serikali kuu ambayo ndio ina dhamana ya kusambaza vifaa tiba baada ya Halmashauri kukamilisha ujenzi wa Zahanati ” Amesema Machela.

Akijibu hoja ya sintofahamu waliyonayo wananchi wa Kiegea kuhusu hatma ya umilki wa ardhi, amesema Baraza la Madiwani limepitisha ya kwamba kwa wananchi walioongezewa maeneo wasitozwe pesa yoyote kwa ongezeko hilo bali wamiliki bure kutokana na uhitaji wa wananchi wasio na uwezo



*Picha mbalimbali za matukio ya ziara ya Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini ya kujifunza namna yauendeshaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo Soko Kuu la Chifu Kingalu na Stendi ya Mabasi Msamvu katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambapo ziara hiyo ilifanyika Machi 03/2023.*
















*Picha za matukio ya kukabidhi Pikipiki 436 kwa Maafisa Ugani Mkoa wa Morogoro zilizotolewa na Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuhakikisha Sekta ya Kilimo Mkoa wa Morogoro inakuwa na tija pamoja na kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ambapo katika tukio hilo Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Rebbeca Nsemwa alikabidhi Pikipiki hizo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Fatma Mwassa.*

## KAMATI NDOGO YA MAZINGIRA MANISPAA YA MOROGORO YAFANYA ZIARA, DIWANI KILONGO ATOA MKONO WA POLE KWA WANGA WA MAFURIKO

Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Mazingira Manispaa ya Morogoro, Mhe. Hamisi Kilongo, akiongozana na Wajumbe wa Kamati hiyo, wamefanya ziara ya kamati hiyo ambapo katika ziara walitembelea Kata ya Kihonda Maghorofani pamoja na Kata ya Kihonda.

Ziara hiyo imefanyika Januari 18/2023, ambapo lengo la ziara hiyo ni kuangalia changamoto za usafi katika Kata ya Kihonda Maghorofani baada ya kupata malalamiko juu ya mdhabuni wa usafi Kata hiyo na kutembelea Kata ya Kihonda kuangalia eneo lililopita mkondo wa maji unaosababisha mafuriko wakati wa mvua Kata ya Kihonda.

Katika Kuona namna gani ya kutatua kero ya usafi Kata ya Kihonda, Kamati ilimtaka madhabuni wa usafi wa Kata ya Kihonda Maghorofani ambaye ni Kajenjere kuonesha taarifa za madeni wanazowadai wananchi lakini kufanyia kazi malalamiko ya wananchi katika uzoaji wa taka kwa wakati.

"Tumepokea malalamiko kutoka kwa Diwani wa Kata hii kufuatia wananchi kumlalamikia ucheleweshwaji wa uzoaji wa taka, sasa kama kamati kwanza tumemtaka mdhabun Kajenjere kuyafanyia kazi malalamiko ya wananchi, lakini kutuletea taaria ambazo wanadai kuwa wananchi wa Kata hiyo wanadaiwa baada ya hapo sasa tutakaa kuona namna bora ya sisi na wao jinsi ya kufanya kazi, tunataka Mji wetu uwe safi, taka zikizagaa hvyo zitaleta magonjwa ya mlipuko, " Amesema Mhe. Kilongo.

Kwa upande wa Mjumbe wa Kamati hiyo,ambaye ni Diwani wa Kata ya Mbuyuni, Mhe. Samwel Msuya, amewataka wadhabuni wa usafi pamoja na vikundi kazi vilivyopewa dhamana ya usafi wafanye kazi kwa kuzingatia mikataba waliyosaini ili kuhakikisha Mji wetu unakuwa safi.

Katika hatua nyengine, Mhe. Kilongo ambaye ni Diwani wa Kata ya Kihonda, alifika Kata ya Kihonda Januari 18/2023 akiongozana na Wajumbe wa Kamati ndogo ya Mazingira kuwaona wahanga na kutoa Msaada wa Unga wa Sembe ikiwa ni jitihada za kuwasaidia wananchi hao walio atharikika sana na mafuriko na kupotelewa na vitu na kukosa mahitaji muhimu ya kibinadamu.

# JIJI LA ARUSHA LAPONGEZA MANISPAA YA MOROGORO KWA UTEKELEZAJI BORA WA MIRADI YA MAENDELEO.

Halmashauri ya Jiji la Arusha imetoa pongezi kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa utekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo kwa ajili ya Wananchi wa Manispaa hiyo.
Pongezi hizo zimetolewa Januari 18/2023 wakati wa ziara ya Jiji hilo la kufanya ziara ya kujifunza namna ya uendeshaji wa miradi mikubwa ya maendelea ikiwemo Soko kuu la Chifu Kingalu na stendi ya Mabasi ya Msamvu.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Meya wa Jiji la Arusha, Mhe. Maxmillian Iraghe, amesema kuwa kitendo cha Manispaa ya Morogoro kutekeleza miradi ya maendeleo ni moja ya hatua kubwa ya kuhakikisha ya kwamba wananchi wanapata huduma bora “Tunawapongeza sana Manispaa ya Morogoro kwa kutekeleza miradi hii mikubwa ya maendeleo, soko kuu pamoja na kituo cha mabasi cha kisasa Msamvu ni hatua kubwa mno mmeifanya, tumeona mmefanikiwa jinsi ya kuwapanga wafanyabiashara wadogo wadogo, sisi tumekuja kujifunza kutoka kwenu na tunakwenda kutekeleza katika Halmashauri yetu.” Amesema Mhe. Iraghe.

"Hongereni Manispaa ya Morogoro kwa kuwa na miradi ya Kimkakati, tumejifunza mengi lakini kubwa, ni utaratibu wa uendeshaji wa Soko , utaratibu huu ni rahisi sana kupelekea kutokuwepo kwa migogoro baina ya wafanyabiashara na Viongozi" Ameongeza Mhe. Iraghe.
Kwa upande wa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro , Mhe. Paschal Kihanga, amepongeza Jiji la Arusha kwa hatua waliochukua ya kufanya ziara kwani Manispaa ya Morogoro imekuwa chuo cha mafunzo hususani katika miradi ya kimkakati.
Aidha kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Jeremiah Lubeleje, amesema kuwa uamuzi walioufanya wa kujenga kituo cha kisasa cha mabasi Msamvu ni chanzo kikubwa cha mapato kwenye Halmashauri.



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, (kushoto) akiwaonesha Madiwani wa Jiji la Arusha muonekano wa kituo cha Mabasi Msamvu kinachomilikiwa na Manispaa ya Morogoro (aliyevaa shati jeupe) ni Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha, Mhe. Maxmillian Iraghe.*




*Muonekano wa ndani wa Kituo cha Mabasi Msamvu kinachomilikiwa na Manispaa ya Morogoro.*

*Picha za matukio ya Kongamano la Mjadala wa Familia ,kongamano lililoandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la WICOF Chini ya Mkurugenzi wake Mwajabu Dhahabu katika Ukumbi wa Kilakala Soko Kuu la Chifu Kingalu Morogoro Februari 25/2023 ambapo mgeni rasmi wa Kongamano hili alikuwa Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Faraja Maduhu.*











*Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro , Fides Likopero, (katikati), Afisa Lishe Manispaa ya Morogoro, Jacqueline Mashurano (kulia), na Mwakilishi wa Watendaji wa Kata ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Mafiga , Amina Saidi, wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kusaini mkataba wa upangaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa shughuli za Lishe kwenye maeneo ya kata zao.*

# WATENDAJI WA KATA MANISPAA YA MOROGORO WASAINI MKATABA WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA AFUA ZA LISHE

Maafisa Watendaji wa kata 29 Manispaa ya Morogoro ,wamesaini mkataba wa upangaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa shughuli za Lishe kwenye maeneo ya kata zao, huku wakitakiwa kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia malengo makuu , viashiria na vigezo vilivyoainishwa kwenye makataba huo.

Maafisa hao wamesaini mkataba huo baina yao na Mkurugenzi Januari 24/2023 ,katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi Kuu ya Manispaa.

Mkataba huo wa lishe ni hatua ya muendelezo wa uingiaji wa mikataba ya usimamizi wa shughuli za afua za lishe kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, wilaya na na hatimaye ngazi ya kata na Mitaa .

Akizungumza wakati wa zoezi la utiaji saini mikataba hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro , Fides Likopero, ameweka wazi kuwa, mkataba huo una malengo makuu mawili ikiwa ni kufanikisha suala la kuboresha hali ya lishe na kupunguza athari za utapiamlo na kuhakikisha jamii inashiriki ipasavyo kupanga, kutekeleza na kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa halmashauri wa afua za lishe.

Likopero , amesema kuwa kwa kuzingatia malengo hayo Maafisa Watendaji ambao ni wasimamizi wapaswa kufanya kazi hiyo kwa weledi kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, kulingana na vigezo na viashiria vilivyoanishwa kwenye mikataba .

"Kila mtu anafahamu umuhimu wa afya bora katika maisha ya binadamu na ujenzi wa Taifa, Serikali imewapa jukumu hili muhimu, nendeni mkalitekeleze kwa umakini mkubwa kulingana na makubaliano, kama kuna changamoto tushirikishane kwa wakati ili kwa pamoja tufikie malengo yaliyokusudiwa na serikali". Amesema Likopero.

Naye Afisa Lishe Manispaa ya Morogoro, Jacqueline Mashurano, amefafanua kuwa, Mkataba wa lishe unawataka Maafisa Watendaji wa Kata kuhakikisha wanashirikiana na Maafisa Watendaji wa Mitaa , kufanya kazi hiyo pamoja na kufanya tathmini na kutoa ripoti ya utekelezaji kwa kila mwezi.

"Lishe duni inanikusababisha umasikini katika Taifa kwani hakutakuwa na Jamii inayoweza kujituma kwa kufanya kazi kutoakana na watu wengi kuathiriwa na utapiamlo, viongozi wenzangu tupambane kutokomeza utapiamlo katika maeneo yetu,,ili kuwa na watu wenye afya bora"Amesema Mashurano.

Naye Afisa Mtendaji wa Kata ya Mafiga ,kwa niaba ya Watendaji wenzake, amesema watakwenda kufanyia kazi maelekezo yote kama yalivyo malengo yake kwa kuzingatia vigezo na viashiria vilivyoainishwa kwenye mkata, ikiwa ni pamoja na kuifanya agenda ya kudumu kwenye vikao vyote vya kisheria.

Ifahamike kuwa mkataba wa Lishe ni mkakati wa Kitaifa ambao ulisainiwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na kusainiwa na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini.



Watendaji wa Kata wakiwa katika picha ya pamoja katika zoezi la kusaini mkataba wa upangaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa shughuli za Lishe kwenye maeneo ya kata zao.

## MEYA KIHANGA AKUNWA NA UTENDAJI KAZI WA WATAALAMU MANISPAA YA MOROGORO.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, amefurahishwa na kazi nzuri inayofanywa na Wataalamu wa Manispaa ya Morogoro katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

Kauli hiyo, ameitoa katika kikao cha Kawaida cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano Ofisi Kuu ya Manispaa Februari 08/2023.

Akizungumza katika Baraza hilo, Mhe. Kihanga, amesema miradi inayotekelezwa na Manispaa kupitia wataalamu ni mizuri na imeonesha na kuzingatia thamani ya fedha.

"Wataalumu wetu wanafanya kazi kubwa, tuwapongeze, miradi inakwenda vizuri, tumeona madarasa ya Pochi la Mama yamekamilika kwa wakati na watoto wetu wanasoma vizuri, endeleeni kuchapa kazi, tuna ndoto ya kuwa Jiji, bila kuwa na miradi ya uhakikka ndoto yetu itachelewa kutimia" Amesema Kihanga.

Katika hatua nyengine, amewataka Madiwani katika kuelekea Bajaeti ya fedha ya mwaka 2023/2024, wajipange vizuri na kutafakari kubuni miradi mikubwa ambayo itaongeza mapato ya Halmashauri.

" Mwaka 2015/2020 Baraza la Madiwani lilifanya kazi kubwa ya kuibua vyanzo vikubwa vya mapato hadi tunafikisha makusanyo ya Bilioni 12 sio kazi ndogo, ni kazi yetu sisi tuliopo tuhakikishe tunabuni vyanzo vipya na vikubwa vitakavyo tuhakikishia makusanyo makubwa ya mapato , muda mnao Madiwani mjipange kuja na mikakati mikubwa tunapoelekea Bajeti ya fedha ya mwaka 2023/2024" Ameongeza Mhe. Kihanga.

Mwisho,amewashukuru Wananchi wa Manispaa ya Morogoro kwa kuendelea na moyo wa ujenzi wa Taifa kwa kuchangia michango mbalimbali ya Maendeleo, hususani katika Ujenzi wa Maboma ya Shule



***Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhe. Pascal Kihanga, akizungumza katika kikao cha Kawaida cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano Ofisi Kuu ya Manispaa Februari 08/2023.***



***Afisa Elimu vifaa na takwimu elimu Msingi, Amna Kova, (watatu kulia) akiendesha zoezi la ugawaji wa vitabu kwa Waalimu wa shule za Msingi kwa ajili ya kuwafundishia wanafunzi.***

## ZAIDI YA VITABU 45,486 VYA KABIDHIWA KWA WAALIMU WA SHULE ZA MSINGI MANISPAA YA MOROGORO.

Manispaa ya Morogoro imegawa vitabu 45,486 kwa Waalimu wa shule za Msingi kwa ajili ya kuwafundishia wanafunzi.

Vitabu hivyo vimetolewa februari 05/2023 katika Ofisi Kuu ya Manispaa ambapo kwa kila shule walikuwepo wawakilishi kwa ajili ya kupokea vitabu hivyo.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi vitabu hivyo, Afisa Elimu Msingi Manispaa ya Morogoro , Chausiku Masegenya, amewataka waalimu na wanafunzi kutumia vitabu hivyo kwa kuvitunza kwa lengo la kutumika kwa muda mrefu wakati wa masomo yao na kuamini kwamba vitabu hivyo vitaleta ufanisi katika kukuza uelewa wa wanafunzi na kuweza kufanya vizuri katika masomo yao.


Aidha, Chausiku, amewataka walimu wa shule kufuatilia kwa makini wanafunzi wote watakaopatiwa vitabu hivyo ili visipotee.

Miongoni mwa vitabu hivyo ni vitabu vya kiada darasa la kwanza na la pili 23,086, vitabu vya hadithi vyenye ukubwa wa A4 vikiwa 20,175 na vitabu vya hadithi vyenye ukubwa wa A3 vikiwa 2,225.

" Tunaishukuru Serikali chini ya Rais wetu , Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutupatia vitabu hivi, tunaamini lengo la Serikali kutupatia vitabu hivi ni kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa waalimu ili kukuza viwango vya elimu , tunaomba waalimu mkavitunze vizuri" Amesema Masegenya.

Kwa upande wa Afisa Elimu vifaa na takwimu elimu Msingi, Amna Kova, amewataka waalimu kuvitunza vitabu hivyo ili viendelee kusaidia vizazi vijavyo huku akiwataka waalimu kuona umuhimu huo na kusimamia kwa faida ya kuongeza tija katika ufundishaji.





*Picha za Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Morogoro (DCC) kilichofanyika Katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi Kuu Manispaa ya Morogoro Februari 10/2023 ambapo kikao hicho kiliongozwa na Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro , Ruth John akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro.*











***Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Rebeca Nsemwa, akizungumza katika Mkutano Maalum wa Baraza la Madiwani la kupitisha mpango na Bajeti ya Manispaa ya mwaka wa fedha 2023/2024 uliofanyika Februari 20, 2023.***

# DC NSEMWA AWATAKA MADIWANI MANISPAA YA MOROGORO KUBUNI VYANZO VIPYA VYA MAPATO.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Rebeca Nsemwa , amewataka Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuboresha vyanzo vilivyopo ili kuwezesha Halmashauri kuweza kuongeza uwezo wa kujitegemea kwa mapato ya ndani ya Halmashauri.
DC Nsemwa, ameyasema hayo Februari 08/2023 katika Mkutano wa Kawaida wa Baraza la Madiwani uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi Kuu Manispaa ya Morogoro.
Aidha,a mesema kuwa Halmashauri ikiboresha mapato itasaidia kutoa huduma za jamii kwa wananchi ikiwemo afya, elimu, Maji pamoja na kuongeza viwango vya mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake.
Hata hivyo, amewataka Waheshimiwa Madiwani kutenga muda wa kupitia vyanzo vyote vya mapato ili kuweka usimamizi mzuri ambao utapelekea ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.
Pia, amesema kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani lazima uendane na nidhamu ya matumizi ya fedha kwa hiyo ni jukumu la Baraza la Madiwani kusimamia na kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa katika vyanzo vya ndani yanatumika ipasavyo.
“Niombe sana Waheshimiwa Madiwani na Watumishi hakikisheni fedha zinazokusanywa kupitia katika miradi yote zisitumike zikiwa mbichi, bali zinatakiwa kupelekewa benki na kutumika kwa kufuata utaratibu mzuri na ulio sahihi kisheria , “ Amesema DC Nsemwa.
Kwa upande wa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini, Fikiri Juma, amewataka madiwani hao kuwa na umoja na mshikamano katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowasilishwa kwao kutoka kwa wananchi ili kuweza kuzitatua na kuzijadili kwa pamoja.



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
OFISI YA MKURUGENZI
S.L.P 166
**MOROGORO TANZANIA**
(C) 2023